



## **Wilaya ya Shule ya Steelton-Highspire**

**McKinney-Vento**

**Kitabu cha Mwongozo cha Wazazi/Walezi**



**250 Reynders Street**

**Steelton, PA 17113**

**717-704-3800**

**[www.shsd.k12.pa.us](http://www.shsd.k12.pa.us)**



## **Yaliyomo**

|                                                  |    |
|--------------------------------------------------|----|
| Programu ya McKinney Vento.....                  | 3  |
| Fasili ya Ukosefu wa Makazi.....                 | 3  |
| Hali ya Maisha chini ya Sheria.....              | 3  |
| Haki za Wanafunzi Chini ya Sheria.....           | 4  |
| Dalili Mbaya za Ukosefu wa Makazi.....           | 4  |
| Vijana Wasio na Msindikizaji.....                | 4  |
| Majukumu ya Mawasiliano ya Wasio na Makazi ..... | 6  |
| Mchakato wa Migogoro wa McKinney-Vento.....      | 7  |
| Rasilimali za McKinney-Vento.....                | 10 |



## **Programu ya McKinney-Vento**

Sheria ya Usaidizi kwa Wasio na Makazi ya McKinney-Vento ni sheria ya serikali kuu inayolenga kuhakikisha uthabiti wa kielimu kwa watoto na vijana wasio na makazi. Agizo hili linatimilizwa kupitia afisa uhusiano wa wasio na makazi. Msimamizi au Mkurugenzi Mtendaji anampa nafasi mtu ambaye ana uwezo wa kutekeleza majukumu/maagizo chini ya Sheria.

### **Fasili ya Ukosefu wa Makazi:**

Chini ya Sheria ya Usaidizi kwa Wasio na Makazi ya McKinney-Vento, watoto na vijana ambao hawana makazi ya kudumu, ya kawaida au ya kutosha usiku watachukuliwa kuwa hawana makazi.

- Kudumu: Makazi ya kudumu ni yale yasiyo ya kuhama hama, ya muda wote na ambayo hayabadiliki.
- Kawaida: Makazi ya kawaida ni yale ya desturi, ya kila siku na yanayotumiwa kila mara.
- Kutosha: Makazi ya kutosha yanafaa kwa makazi ya binadamu. Yanakidhi mahitaji ya kimwili na kisaikolojia ambayo kwa kawaida hutimizwa mazingira ya nyumbani.

### **Hali za maisha chini ya Sheria ni hujumuisha:**

- Makao na programu za nyumba za mpito
- Magari, bustani na makazi duni
- Kuishi kwenye makazi ya wengine kutokana na matatizo ya kiuchumi au upotevu wa makazi
- Hoteli, moteli au kambi kwa sababu ya ukosefu wa nyumba nyingine zinazofaa
- Vijana wahamiaji wanaoishi katika mojawapo ya mazingira tajwa hapo juu

Watoto na vijana wanaoishi katika mojawapo ya mazingira tajwa hapo juu kutokana na tukio ambalo liliwalazimu kuondoka nyumbani kwao watafuzu kupata ulinzi wa McKinney-Vento.



### **Haki za Wanafunzi Chini ya Sheria:**

- Haki ya kuendelea katika shule ya mwanzoni, shule waliyosoma kabla ya kupoteza makazi au shule ambayo waliandikishwa kwa mara ya mwisho.
- Haki ya kuhamishwa katika shule ya makazi.
- Haki ya kuandikishwa mara moja hata kama hawana hati zinazohitajika kama vile rekodi za chanjo au uthibitisho wa makazi.
- Haki ya kupewa usafiri wa kwenda na kurudi shule ya mwanzoni kwa muda wa ukosefu wa makazi au kwa mwaka mzima wa masomo baada ya kupata makazi ya kudumu.
- Haki ya kuwekwa kwenye programu ya bila malipo ya kifungua kinywa na chakula cha mchana shuleni.
- Usaidizi wa ada/ faini ikiwemo ziara za kimasomo, elimu ya viungo, ada za maabara, shughuli za ziada zinazofadhiliwa na shule na ada nyinginezo za shule.
- Usaidizi wa kupata vitu vya kujifunzia ikiwemo vifaa vya shule.
- Usaidizi wa kuunganishwa na mashirika ya huduma za kijamii katika jumuiya.

### **Dalili Mbaya za Ukosefu wa Makazi:**

- Mahudhurio katika shule kadhaa/ shule za awali
- Zaidi ya familia moja katika anwani moja
- Anwani za hoteli, moteli au makao (shelter)
- Usiri au hasira akiulizwa kuhusu anwani au hali ya sasa ya maisha
- Anashinda kutoa anwani ya sasa
- Kulala darasani
- Mavazi yasiyoendana na hali ya hewa
- Njaa na kulimbikiza chakula
- Tabia ya kutafuta kujionesha
- Kukosa masomo kwa muda mrefu

### **Vijana Wasio na Msindikizaji**

Chini ya Sheria ya McKinney-Vento, kijana asiye na msindikizaji anaelezewa kama mtoto au kijana ambaye hayupo chini ya uangalizi wa kimwili wa mzazi



au mlezi na hana makazi ya kudumu, ya kawaida au ya kutosha usiku. Kijana asiye na msindikizaji hahitaji tukio la kustusha ili astahiki huduma za McKinney-Vento. Kijana asiye na makazi anapotambuliwa, wilaya itafuata taratibu tajwa hapo juu lakini pia itajumuisha mambo yaliyoorodheshwa hapa chini.

- Baada ya utambulisho na rufaa kwa afisa uhusiano wa wilaya wa wasio na makazi, afisa uhusiano huyo atathibitisha hali ya kijana asiye na msindikizaji ya kijana huyo.
- Mwanafunzi ataandikishwa mara moja katika wilaya anayoishi au atabaki katika wilaya anayotoka kama mwanafunzi wa kujitegemea. Hii ina maana kuwa vijana wasio na msindikizaji wanaweza kuandikishwa bila mzazi au mlezi.
- Taratibu za wilaya za vijana wasio na msindikizaji ni kama ifuatavyo:
  - Ikiwa mwanafunzi ana miaka 18 au zaidi na ni mwanafunzi wa elimu ya kawaida, atakuwa na haki ya rekodi yake ya elimu na kusaini nyaraka zote kama mwanafunzi wa kujitegemea.
  - Ikiwa mwanafunzi ana miaka chini ya 18 au ana IEP, wazazi au walezi watakuwa na haki zao za elimu chini ya FERPA.
  - Ikiwa mwanafunzi ana IEP na hakuna ushiriki wa wazazi katika elimu yake, mzazi mbadala au mlezi mtu mzima atakabidhiwa kwa mwanafunzi.
  - Ikiwa mwanafunzi ana miaka chini ya 18, ni mwanafunzi wa elimu ya kawaida na hana ushiriki wa wazazi, msimamizi wa wilaya au mlezi mtu mzima atapewa jukumu la kumsaidia mwanafunzi huyo katika maamuzi ya kielimu.
  - Pale mlezi mtu mzima anapokabidhiwa kijana, mtu huyu atajaza fomu ya mlezi wa wilaya.
- Afisa uhusiano wa wilaya atasaidia katika ongezeko la alama (credit accrual) na kutoa ushauri wa chuo na kazi.
- Afisa uhusiano wa wilaya utatoa barua ya uthibitisho ya vijana wasio na makazi ambao hawana msindikizaji kwa madhumuni ya usaidizi wa kifedha wa chuo.

Marejeleo



ECYEH Sample Procedures-

[https://drive.google.com/file/d/1iVxkhf\\_hQQYhH4sD5vl43x9zZ09o2jVC/view](https://drive.google.com/file/d/1iVxkhf_hQQYhH4sD5vl43x9zZ09o2jVC/view)

NCHE Determining Eligibility for MKV- [https://ncche.ed.gov/wp-content/uploads/2018/10/det\\_elig.pdf](https://ncche.ed.gov/wp-content/uploads/2018/10/det_elig.pdf)



### **Majukumu ya Afisa Uhsuano wa Wasio na Makazi:**

- Watoto na vijana wasio na makazi wanatambuliwa na wafanyakazi wa shule kupitia shughuli za uhamasishaji na uratibu na vyombo vingine.
- Watoto na vijana wasio na makazi huandikishwa mara moja na kupata ufikio kamili wa programu ya elimu wakiwa na au wasipokuwa na hati muhimu za kuandikishwa.
- Watoto na vijana wasio na makazi wanaweza kufikia programu sawa za elimu, ikiwemo programu za elimu ya awali, kama wanafunzi wenye makazi ndani ya shirika mahalia la elimu (LEA).
- Familia zisizo na makazi na watoto na vijana wasio na makazi hupokea rufaa kwa mashirika ya nje ikiwemo matibabu, meno, afya ya akili, nyumba na huduma nyingine zinazofaa.
- Wazazi/walezi wa watoto na vijana wasio na makazi wanafahamishwa kuhusu fursa za elimu na zinazohusiana nazo zinazopatikana kwa watoto wao na wanapewa fursa stahiki za kushiriki katika elimu ya watoto wao.
- Notisi ya umma kuhusu haki za kielimu za watoto na vijana wasio na makazi inasambazwa katika maeneo yanayotembelewa na wazazi au walezi wa watoto na vijana kama hao, na vijana wasio na wasindikizaji, ikiwemo kitabu cha wanafunzi na tovuti ya wilaya. Taarifa zitakuwa katika namna na muundo unaoeleweka kwa wazazi, walezi na vijana wasio na wasindikizaji.
- Migororo ya uandikisho inasuluhishwa kwa mujibu wa matakwa ya Idara ya Elimu ya Pennsylvania (PDE).
- Mzazi au mlezi wa mtoto au kijana asiye na makazi, na kijana yeyote asiye na msindikizaji, anafahamishwa kikamilifu kuhusu haki yake ya usafiri. Usafiri utapangwa bila kuchelewa.
- Wafanyakazi wa shule wanaotoa huduma chini ya ibara hii ndogo huendelezwa kitaaluma na kupewa usaidizi mwingine.
- Vijana wasio na msindikizaji watashughulikiwa moja kwa moja kama wanafunzi wa kujitegemea.



## **Mchakato wa Migogoro wa McKinney-Vento**

Kwa mujibu wa Sheria ya McKinney-Vento, kila jimbo lazima liandae taratibu za utatuzi wa haraka wa migogoro kuhusu uandikisho wa kielimu wa watoto na vijana wasio na makazi. 42 USC §11432(g)(1)(C). Jimbo lazima lihakikishe kwamba Mashirika Mahalia ya Elimu (LEA) yanatii matakwa yaliyoainishwa katika Sheria ya McKinney-Vento ikiwemo kuhakikisha uandikisho wa mara moja, kutoa notisi ya maandishi kwa familia kuhusu uteuzi wa shule, maamuzi ya uandikisho na kutoa uandikisho na usubirisho katika shule anayochagua wakati mgogoro unatatuliwa. 42 USC §11432(g)(2)(A). Idara ya Elimu ya Pennsylvania (PDE) imeandaa taratibu zifuatazo ili kusimamia utatuzi wa migogoro kuhusu uandikisho, uteuzi wa shule, hali ya kutokuwa na makazi na malalamiko ya kutofuata matakwa ya kisheria yanayohusu elimu kwa watoto na vijana wasio na makazi:

**Mgogoro wa Ngazi ya 1- Mgogoro unaweza kuibuliwa na LEA.**

Ikiwa mgogoro utatokea kuhusu uteuzi au uandikisho wa shule, mtoto au kijana husika lazima akubaliwe mara moja katika shule anayotaka kujiandikisha, akisubiri usuluhishi wa mgogoro 42 USC§11432(g)(3)(E)(i). PDE inapendekeza kwamba mzazi, mlezi au kijana asiye na msindikizaji anayeanzisha mgogoro awasiliane na afisa uhusiano wa LEA wa watu wasio na makazi haraka iwezekanavyo baada ya kupokea taarifa ya mgogoro huo. Ikiwa mtu anayeanzisha mgogoro hatawasiliana na afisa uhusiano wa LEA moja kwa moja, LEA itawajibika kuwasiliana na afisa uhusiano wa LEA kuhusu mgogoro huo haraka iwezekanavyo na kuelekeza familia au kijana anayehusika kwa afisa uhusiano huyo.

Afisa uhusiano wa LEA atahakikisha mtoto au kijana ameandikishwa mara moja, ataelezea mchakato wa kutatua migogoro kwa familia na kuisaidia kuutumia 42 USC §11432(g)(3)(E)(iii). LEA itatoa uamuzi wa maandishi wa mgogoro ndani ya siku 20 za kazi baada ya afisa uhusiano wa LEA kuarifiwa mgogoro huo. Uamuzi huo utatolewa kwa mzazi, mlezi au kijana asiye na msindikizaji na utaeleza msingi wa uamuzi huo na kumshauri mzazi, mlezi au kijana juu ya haki ya kukata rufaa. 42 USC§11432(g)(3)(E)(i).



KUMBUKA: LEA inapaswa kutumia na kutunza nakala za fomu ya "Notisi ya Ulinzi wa Taratibu" ya PDE ambayo inahakikisha kwamba LEA zote (a) zitafahamisha familia kuhusu msingi wa uamuzi wao kuhusiana na uandikisho au uteuzi wa shule; (b) zitaifahamisha familia kuhusu haki yao ya kubaki katika shule wanayochagua wakisubiri kusuluhishwa kwa mgogoro na (c) zitaelezea taratibu za kupinga uamuzi wa LEA.

Mgogoro wa Ngazi ya 2- Malalamiko yanaweza kuwasilishwa kwa mratibu wa McKinney-Vento. Ikiwa mzazi, mlezi au kijana asiye na msindikizaji hajaridhika na uamuzi wa LEA kuhusu mgogoro au angependa kuibua suala lolote la kutozingatia Sheria ya McKinney-Vento, anaweza kuwasilisha malalamiko au kukata rufani kupitia mratibu wa eneo au kanda au jimbo wa McKinney-Vento. (Angalia orodha ambatishwa yenye taarifa za mawasiliano za waratibu wote wa McKinney-Vento wa Pennsylvania). Badala ya kuwasilisha rufaa kwa mratibu wa McKinney-Vento, mzazi, mlezi au kijana asiye na msindikizaji anaweza kuchagua kukata rufani dhidi ya uamuzi wa LEA moja kwa moja kwa mahakama yenye mamlaka. Ushiriki katika utaratibu wa kukata rufani hauhitajiki kabla ya kuchukua hatua za kisheria.

Wazazi, walezi, na vijana wasio na msindikizaji wanapaswa kujulishwa kwamba wanaweza kutoa hati za maandishi au za mdomo ili kuunga mkono msimamo wao; na

Wazazi, walezi, na vijana wasio na msindikizaji wanapaswa kupewa fursa ya kupinga madai ya mfumo wa shule.

Mratibu wa kanda au eneo ambaye malalamiko au rufaa inawasilishwa kwake lazima amjulishe mratibu wa jimbo mara moja. Baada ya kuarifiwa, mratibu wa serikali atapitia malalamiko au rufani na kukabidhi kwa mratibu wa eneo au kanda ili yatatuliwe. Mratibu ambaye rufaa imewasilishwa kwake anaweza kuwasiliana, kuhoji na kukubali hati kutoka kwa mtu yeyote au LEA husika, na atatoa uamuzi wa maandishi ndani ya siku 20 za kazi baada ya malalamiko au rufani kufikishwa kwake. Uamuzi huo utatolewa kwa LEA na mzazi, mlezi au kijana asiye na msindikizaji ambaye anahusika. Mtoto au kijana ataendelea kuandikishwa katika shule ambayo anataka kuandikishwa hadi malalamiko au rufani itakapotatuliwa au hadi uamuzi kutoka kwa mratibu wa McKinney-Vento



utakapopokelewa.

Ikiwa uamuzi hauwezi kufikiwa au kukubaliwa katika ngazi ya mratibu wa eneo, mgogoro huo utapelekwa kwa mratibu wa jimbo kwa ajili ya kusuluhishwa. Mratibu wa serikali atapitia taarifa zote na kuwahoji watu wote wanaohusika. Ofisi ya Mshauri Mkuu (OCC) itajumuishwa katika mchakato wa usuluhishi inapohitajika. Ikiwa huduma za upatanishi zinahitajika, mratibu wa jimbo atasaidia katika upatanishi na pia anaweza kuwaalika wale wanaohusika ili mgogoro huo usuluhishwe wakati wowote katika mchakato kupitia Programu ya Utatuzi wa Migogoro (DRP) inayoendeshwa na Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Jumuiya ya Madola (OGC). [Programu ya Utatuzi wa Migogoro ya OGC](#) ni mchakato usio rasmi na wa hiari ambapo mpatanishi mwenye mafunzo husaidia kufikia suluhu inayokubalika na pande zote.

Kushiriki katika upatanishi si kuondolewa kwa haki ya kufungua kesi wala kushiriki katika upatanishi kunahitajika kabla ya kuchukua hatua za kisheria.

KUMBUKA: Mzazi, mlezi au kijana asiye na msindikizaji anaweza kuwasilisha malalamiko kwa mratibu wa eneo, kanda au jimbo wa McKinney-Vento kwenye fomu ya malalamiko iliyoambatishwa. Hata hivyo, si lazima kutumia fomu iliyoambatanishwa. Mgogoro wowote ulioibuliwa na familia au vijana wasio na makazi kuhusu uandikisho shuleni au haki nyingine yoyote chini ya Sheria ya McKinney-Vento uwe umepokewa kupitia simu, barua au njia yoyote ya mawasiliano utachukuliwa kuwa malalamiko.

<https://www.education.pa.gov/K-12/Homeless%20Education/Pages/DisputeResolutionProcess.aspx>



## Rasilimali za McKinney-Vento

**Sera 251 ya Bodi ya Shule ya SHSD Wanafunzi Wasio na Makazi**

<https://go.boarddocs.com/pa/stlh/board.nsf/public#>

**42 USC SURA YA 119, SURA NDOGO YA VI, Sehemu B: Elimu kwa Watoto na Vijana Wasio na Makazi**

<http://uscode.house.gov/view.xhtml?path=/prelim%40title42/chapter119/subchapter6/partB&edition=prelim>

**PDE BEC- Elimu kwa Vijana Wasio na Makazi**

<https://www.education.pa.gov/Policy-Funding/BECS/uscode/Pages/EducationforHomelessYouth.aspx>

**Mwongozo Usio wa Udhhibiti wa Programu ya Elimu kwa Watoto na Vijana Wasio na Makazi**

<https://www2.ed.gov/policy/elsec/leg/essa/160240ehcyguidance072716.pdf>

**Karatasi ya Mambo Muhimu ya EHYC**

<https://www2.ed.gov/policy/elsec/leg/essa/160315ehcyfactsheet072716.pdf>

**Afisa Uhusiano wa Wilaya**

Afisa Uhusiano wa Ngazi ya Wilaya: Dkt. Samantha Neidlinger,

[sneidlinger@shsd.k12.pa.us](mailto:sneidlinger@shsd.k12.pa.us)

717-704-3800 ext. 3862

Afisa Uhusiano wa Ngazi ya Jengo: Dkt. Sadie Kinnarney,

[skinnarney@shsd.k12.pa.us](mailto:skinnarney@shsd.k12.pa.us)

717-704-3800 ext. 4204

**\*\*Ikiwa wewe na/au familia yako hamna makazi, tafadhali wasiliana nasi kwa kutumia maelezo yaliyo hapo juu haraka iwezekanavyo. Tutafurahi kusaidia!**



### **Mawasiliano Mahalia**

- Orodha ya Afisa uhusiano wa watu wasio na makazi mtandaoni wa Pennsylvania:

<https://directory.center-school.org/homeless>

- Kanda ya ECYEH 2: 610-987-8509 au [www.berksiu.org/ecyeh](http://www.berksiu.org/ecyeh)

### **Rasilimali Mahalia**

- 211

- Muungano wa Watu Wasio na Makazi (Homeless Coalition):

<https://www.berksiu.org/students-families/k-12-education-student-services/ecyeh/resources/>

- Orodha ya makao mtandaoni: <https://directory.center-school.org/homeless/shelter/search>